TANGAZO LA SERIKALI Na. 682 la tarehe 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA MAGULA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Magula ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba P1 yenye majira - nukta 290764.387E, 9279421.439N katika daraja la mto Magula; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kufuata barabara ya Mpanda – Sumbawanga katika uelekeo wa N 28° 00' 50" E kwa umbali wa kilomita 0.764 mpaka alama ya mpaka ya upimaji namba P2 yenye majira – nukta 291123.695E, 9280096N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa N 63° 26' 47" W kwa umbali wa kilomita 0.432 mpaka alama ya mpaka ya upimaji namba P3 yenye majira - nukta 290736.875E, 9280290.116N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa S 27° 58' 41" W kwa umbali wa kilomita 0.677 hadi alama ya mpaka ya upimaji P4 yenye majira – nukta 290418.900E, 9279691.537N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa S 51° 58' 56" E kwa umbali wa kilomita 0.438 kwa kufuata mto Magula hadi ilipoanzia"

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*